

## RIPOTI YA EMISSIONS GAP YA MWAKA WA 2020 UJUMBE MKUU UNAOWASILISHWA

### MASIMULIZI YA KIWANGO CHA JUU:

Ijapokuwa kumekuwa na upunguzaji wa uzalishaji wa kaboniksidi kutokana na janga la korona (COVID-19), ongezeko la joto duniani linaelekea kuwa juu zaidi kwa nyuzijoto 3 katika karne hii— hali itakayofanya kuwa vigumu kufikia malengo ya Mkataba wa Paris ya kudhibiti kiwango cha joto kuwa chini ya nyuzijoto 2 hadi ifikie nyuzijoto 1.5. Hata hivyo, kujimairisha baada ya janga la korona kunaweza kupunguza uzalishaji wa gesi ya ukaa kwa takribani asilimia 25 jinsi inavyotabiriwa katika mwaka wa 2030 ili kuwezesha duniani kufikia viwango vya nyuzijoto 2. Serikali ni sharti zing'ang'ane kuhakikisha kuwa zinatamia nishati isiyochafua mazingira zinapojiimarisha baada ya korona na kuimarisha ahadi zake kabla ya mkutano ujao utakaotokea katika mwaka wa 2021.

**Ijapokuwa janga la korona litasababisha upunguzaji wa uzalishaji wa gesi chafuzi katika mwaka wa 2020, haitawezesha dunia kuwa karibu kufikia malengo ya Mkataba wa Paris ya kudhibiti kiwango cha joto kuwa chini ya nyuzijoto 2 hadi kitakapofikia nyuzijoto 1.5**

- Kiwango cha joto kilikuwa juu zaidi katika mwaka wa 2020 huku kiwango cha mioto maporini, kiangazi, dhoruba na kuyeyuka kwa theluji kikiongezeka.
- Katika mwaka wa 2019 uzalishaji wa gesi ya ukaa, ikijumuisha mabadiliko katika matumizi ya ardhi, iliongezeka na kufikia gigatani za kaboniksidi (GtCO<sub>2</sub>e).
- Uzalishaji wa kaboniksidi unatarajiwa kupungua kwa asilimia 7 katika mwaka wa 2020. Hata hivyo, kwa kipindi cha mda mrefu, hii inamaanishi kuwa ongezeko la joto duniani litapungua tu kwa asilimia 0.01 kufikia mwaka wa 2050.
- Ahadi zilizotolewa na serikali chini ya Mkataba wa Paris, zinazojulikana kama Ahadi Zilizowekwa na Taifa (NDCs), bado hazitoshi kabisa. Makadirio ya uzalishaji wa gesi chafuzi katika mwaka wa 2030 yanaashiria kuwa joto litaongezeka na kufikia nyuzijoto 3.2 katika karne hii, hata ikuwa ahadi zote za NDCs zinazotolewa kwa hiari zitatimizwa.
- Ahadi za kipekee kwenye Mkataba wa Paris zinahitaji kuimarishwa mara tatu zaidi ili kufikia nyuzijoto 2 na kuimarishwa angalau mara tano zaidi ili kufikia nyuzijoto 1.5.

**Janga lililopo ni onyo kutoka kwa mazingira kuwa ni sharti tushughulikie mabadiliko ya tabianchi, uharibifu wa mazingira na uchafuzi wa hewa. Pia, inatoa fursa ya kujijenga tena ili kuwezesha dunia kufikia kiwango cha joto cha nyuzijoto 2.**

- Matumizi ya nishati isiyochafua mazingira wakati wa kujiimarisha baada ya korona yanaweza kupunguza uzalishaji wa gesi chafuzi inayotarajiwa kushuhudiwa katika mwaka wa 2030 kwa asilimia 25 kwa kuzingatia mikakati iyokuwepo kabla ya COVID-19. Hali hii inaimarisha kiwango cha gesi chafuzi itakayopunguzwa kupitia NDCs zinazotolewa kwa hiari, ijapokuwa juhudi zaidi zinahitajika ili kufikia nyuzijoto 1.5 inavyotakiwa.

- Kujiimarisha kwa kutochafua mazingira kunaweza kufanya uzalishaji wa gesi chafuzi katika mwaka wa 2030 kuwa GtCO<sub>2</sub>e 44– kiwango cha uzalishaji kinachoweza kutoa fursa ya asilimia 66 ya kuwezesha kiwango cha joto kuwa chini ya nyuzijoto 2.
- Hatua zinazopaswa kuchukuliwa kwa haraka zinajumuisha kuunga mkono matumizi ya teknolojia na miundo msingi zisizozalisha gesi ya ukaa, kuondoa ruzuku inayotolewa kwa nishati ya visukuku na, kutoruhusu viwanda vipya vya mawe ya makaa, na kutoa masuluhisho yanayojali mazingira – ikijumuisha kuboresha kiwango kikubwa cha ardhi na kupanda miti katika maeneo iliyokatwa.

**Kufikia sasa, kuanza kutumia mikakati ya kujiamarisha ili kuleta mabadiliko ya kutumia nishati isiyochafua mazingira haijatekelezwa mno. Hali hii isipobadilishwa, malengo ya Mkataba wa Paris hayataweza kutekelezwa**

- Takribani robo ya nchi wanachama wa G20 zimetenga fungu la pesa za matumizi, asilimia 3 ya Pato la Taifa (GDP), kuwezesha mikati ya kupunguza uzalishaji wa gesi ya ukaa.
- Nchi nyingi, zimekuwa zikiwekeza kwenye nishati ya kiwango cha juu cha ukaa, ikiashiria hazijawekeza kwenye nishati isiyochafua mazingira, na kwa hivyo kutoweza kuwa na athari kwa uzalishaji wa gesi chafuzi.
- Hata hivyo, bado kuna fursa kubwa kwa nchi kutekeleza sera na miradi ya uzalishaji mdogo wa gesi ya ukaa. Serikali zinapaswa kutumia fursa hii wakati zinapochukua hatua za kukabiliana na korona zinapounda bajeti.

**Idadi inayoendelea kuongezeka ya nchi zinazotoa ahadi ya kutozalisha gesi ya ukaa kabisa kufikia nusu ya karne hii ndiyo sera muhimu mno ya mazingira katika mwaka wa 2020. Ili kuaminika na kutekelezeka, ahadi hizi ni sharti zifanyiwe kazi kwa dharura na kuwa sera dhabiti kwa kutumia mda mdogo na hata kujumuishwa kwenye NDCs.**

- Wakati ripoti hiyo ilipokamilishwa, nchi 126 zinazokadiriya asilimia 51 ya uzalishaji wa gesi ya ukaa duniani, zimeidhinisha kutangaza au kuweka malengo ya kutozalisha gesi hiyo. Iwapo Marekani itaweka mikati ya kutozalisha gesi ya ukaa kufikia mwaka wa 2050, kama ilivyo kwa mipango ya mazingira ya Biden-Harris, kiwango kitaongezeka na kufikia asilimia 63.
- Ijapokuwa malengo ya kutozalisha gesi ya ukaa yanavutia, yanaonyesha pengo kubwa lililopo kati ya kujitolea kuyatekeleza kikamilifu na viwango duni vya ahadi zilizotolewa kwa NDCs.
- Nchi zaidi zinahitaji kuweka mikakati ya kudumu inayoenda sambamba na Mkataba wa Paris, na kutoa ahadi mpya na hata kuimarisha ahadi zilizotolewa chini ya NDCs ili kufikia malengo ya kutozalisha gesi ya ukaa.

**Sekta ya Usafiri wa meli na wa ndege unachangia asilimia 5 ya jumla ya uzalishaji wa gesi chafuzi na ongezeko lake. Nayo pia inahitaji kushughulikiwa**

- Hali ikiendelea jinsi ilivyo, jumla ya uzalishaji wa gesi chafuzi kutokana na safari za kimataifa za meli na ndege una uwezo wa kupunguza uwezo wa kufikia kiwango kinachohitajika kwa kati ya asilimia 60 na asilimia 220 ya gesi ya kabonkisidi kufikia mwaka wa 2050 tukizingatia hali ya kufikia nyuzijoto 1.5.
- Kuimarishwa kwa teknolojia na utendakazi kunaweza kuimarisha ubora wa nishati inayotumiwa kwa usafiri iwapo matuzo yatatolewa. Ila, ongezeko linalokisiwa kutolewa inamainisha kuwa gesi

ya ukaa wala kabonikisidi havitapungua. Sekta hizo zinapaswa kutumia nishati itakazoziwezesha kuepukana na nishati ya visukuku.

- Sera zaidi zinahitajika ili kuwa na mabadiliko ya teknolojia, utendakazi, mahitaji na matumizi ya nishati.

**Hatua dhabiti zinapaswa kujumuisha, utekelezaji, ushawishi na mabadiliko ya matumizi ya bidhaa kwenye sekta binafsi na ya watu binafsi.**

- Takribani thuluthi mbili za uzalishaji wa gesi chafuzi hutoka kwa sekta binafsi, kwa kuzingatia data ya matumizi ya bidhaa. Kila mojawapo ya sekta ya usafiri, ya majumba ya makaazi, na ya chakula, huchangia angalau asilimia 20 ya uzalishaji unaotokana na jinsi tunavyoishi.
- Serikali zinapaswa kusaidia na kushawishi watumizi wa bidhaa kuepukana na bidhaa zilizo na kiwango cha juu cha gesi ya ukaa. Hatua zinazoweza kuchukuliwa ni pamoja na kutumia reli badala ya kutumia ndege kwa safari fupi, matuzo na miundo msingi kuwezesha matumizi ya baisikeli na watu kutumia magari yao na wenzao, kuboresha nishati inayotumika majumbani, kuwekeza kwenye nishati jadidifu na sera za kupunguza uharibifu wa chakula.
- Uzalishaji wa watu wote matajiri ambao ni asilimia moja ya idadi ya watu wote duniani hukadiria zaidi ya maradufu asilimia 50 ya watu maskini zaidi. Matajiri wanapaswa kupunguza uzalishaji wa gesi ya ukaa angalau mara 30 aidi ili kuwezesha kufikia malengo ya Paris.